

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**



*Dar es Salaam*  
*15 Aprili, 2026*

Barua pepe: [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)

**TAARIFA KWA UMMA  
RAIS SAMIA AKUTANA NA UJUMBE WA JUMUIYA YA MADOLA**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amepokea ujumbe maalum kutoka kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, Bi. Shirley Ayorkor Botchwey, uliowasilishwa kwake na Mjumbe Maalum, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Malawi, Mhe. Dkt. Lazarus McCarthy Chakwera, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Ujumbe huo pia umeainisha maeneo ya kipaumbele yanayofuatiliwa na Jumuiya ya Madola, ikijumuisha uwazi na ushirikiano katika tathmini ya matukio yaliyojitokeza wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025, pamoja na kupanua ushiriki wa kisiasa, kuendeleza majadiliano ya vyama na kuimarisha uwajibikaji wa taasisi.

Katika ujumbe wake, Katibu Mkuu Botchwey amesisitiza dhamira ya Jumuiya ya Madola kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuimarisha misingi ya demokrasia, utawala bora na maridhiano ya kitaifa kufuatia matukio yaliyojitokeza wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025.

Ameeleza kuwa Jumuiya ya Madola inaunga mkono juhudi zinazoendelea nchini na iko tayari kusaidia kujenga mazingira ya kisiasa yenye utulivu, ushirikishwaji na kuaminiana kupitia mazungumzo na mageuzi ya taasisi.

Akizungumza wakati wa kupokea ujumbe huo, Rais Dkt. Samia amesema Tanzania inaendelea kushughulikia hali hiyo kupitia taasisi zake, akizitaja hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali, ikiwemo kuunda Tume Huru ya Uchunguzi, kwa lengo la kurejesha utulivu, na kuimarisha uwajibikaji nchini.

Amebainisha kuwa matokeo ya Tume hiyo yataongoza hatua zinazofuata, ikiwemo uwajibikaji, maridhiano na mageuzi ya taasisi, huku Serikali ikiendelea kusimamia mchakato wa maridhiano ikiwemo majadiliano kupitia majukwaa yaliyopo kisheria na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali.



Kwa upande wake, Mhe. Chakwera ameeleza utayari wa Jumuiya ya Madola kuendelea kushirikiana na Tanzania katika juhudi za kuimarisha utawala wa sheria, ushirikiano wa kisiasa na mshikamano wa kitaifa.

Rais Mstaafu Chakwera amehitimisha ziara yake ya kikazi nchini kama Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola kwa lengo la kufanya tathmini ya hali ya kisiasa na mchakato wa maridhiano, ambapo tayari amekwishakutana na wadau mbalimbali wa kisiasa na kitaasisi nchini.



Shaaban Kissu

K.n.y. Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu